KULIKONI NEWSPAPER, JULY 24, 2007 pg. 7.

# Wamarekani wasaidia yatima

**VALENTINE MARC NKWAME**

Arusha

JUHUDI za pamoja kati ya Watanzania na Wamarekani zitawezesha kujengwa kwa nyumba saba za kituo cha watoto yatima mkoani Arusha ambacho kina idadi ya watoto 100.

Mradi wa ujenzi wa kituo hicho hadi sasa umefanikiwa kujenga majengo saba katika kata ya Ngongongare, tarafa ya Ngurdoto, wilayani Arumeru.

Ujenzi huo unafanywa kwa msaada wa shirika la misaada na maendeleo la Kanisa la Kiadventist lenye makao yake makuu mjini Arusha katika kijiji cha Havillah na tayari majengo mawili ambayo yamo kwenye uwanja wa wa chuo kikuu cha Arusha yameshakamilika. Kituo hicho tayari kinatoa hifadhi kwa watoto kwenye majengo mawili na mojawapo limepewa jina la Irene Wallace ambayo ni mama wa Dakta Robet Wallace ambaye ni mwenyekiti wa bodi ya taasisi ya Global Vessels ambayo inashughulika na mradi wa Havilah. Wakurugenzi wengine Frazier Mathis, ambaye ni rais wa shirika hilo, Virginia Mathis, Jason Allen, Felice Brandon, Larry Elliot, Debra Henry, Cecilia Lester, Roger Watson na Elaine Williams, ambao wote wanatoka Marekani , ambapo kwa upande wa Tanzania wajumbe ni Josiaya Tayalli (mwenyekiti), Max Church (mkurugennzi mkazi), Samson Hian, Benard Mambwe, Joseph Mrutu, Lotti Nnko na Sammy Zakayo.

# Uhifadhi maeneo oevu upewe kipaumbele

**SEBASTIAN MRINDOKO**

Rufiji

KIPAUMBELE kidogo kinachotolewa katika kuhifadhi maeneo oevu kama hadhari haitachukuliwa ipo hatari ya maeneo hayo kutoweka.

Hadhari hiyo ilitolewa na Mkurugenzi mkazi wa Shirika la Kuhifadhi wa Maliasili duniani nchini IUCN Bw. Abdulrahman Issa, kwenye warsha ya siku moja iliyofanyika mwishoni mwa wiki katika kijiji cha Mtanza-Msona wilayani Rufiji Mkoa wa Pwani.

Warsha hiyo ilikuwa na lengo la kujenga uelewa kuhusu umuhimu wa kuhifadhi maeneo oevu ambapo mkurugenzi huyo alitoa changamoto inayotaka wapanga sera kutoa kipaumbele kwa maeneo hayo.



Wakazi wa Dar es Salaa wakiwa wamebeba mifuko iliyosheheni chupa tupu za plastiki katika eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana.

PICHA/JOHN BADI

Wakati maamuzi yanapofanywa juu ya mafungu ya uwekezaji au usimamizi wa ardhi na mali asili ni mara chache kipaumbele kinatolewa kwa maeneo yenye thamani kibaiolojia, kiekolojia maendeleo au uchumi wa maeneo oevu.

Aidha alisema kuwa wapanga sera hao wamekuwa hawana uelewa wa athari zinazoweza kutokea kutokana na uharibifu wa maisha ya kiuchumi na vidokezo vya kupambana na umasikini.

Hata hivyo mamlaka ya usimamizi wa maeneo oevu imefanya juhudi kidogo katika kuelezea muunganiko uliopo kati ya hali ya umasikini na maisha kwa ujumla katika shughuli za uhifadhi.

Kufuatana na na yaliyojitokeza katika katika huduma na bidhaa zinazotokana na maeneo oevu ni muhimu hususani kwa jamii ambazo zimegubikwa na umasikini zikiwwa zimekosa njia mbadala za kupata kipato na chakula na ambao pia hawapiti mahitaji muhimu ya msingi.

Kwa mujibu wa Tathimini ya Milenia ya Mfumo wa ekolojia wa mwaka 2005, baioanuai ya sehemu oevu za ndani zimekuwa kwenye hali mbaya kuliko ilivyo kwa maeneo mengine ambako inakadiriwa kuwa asilimia 50 ya maji mengi kwenye maeneo ya ndani hupotea achilia mbali yale yaliyopo kwenye maziwa makubwa ambayo hupotea kwa kiasi kikubwa zaidi.

Uharibifu wa maeneo hayo na kupotea kwa maji ni tishio kubwa kwa maendeleo na malengo ya kuhifadhi na atahari isiyopimika kwa jamii masikini duniani.

Licha ya kutumia mbinu tofauti katika kutathimini maeneo oevu kibaiolojia. Kiuchumi na kwa thamani ya mahitaji ya jamii ukweli unabakia kuwa kuna ukosefu mkubwa wa mbinu za kutathimini muunganiko uliopo kati ya maeneo hayo kiafya na kiuchumi.

Hata hivyo Mkurugenzi huyo aliipongeza jamii za vijiji vya Mtanza-Msona kwa ushirikiano wao katika miradi ya kuimarisha maeneo oevu ili kuimarisha maeneo hayo kwa faida ya jamii masikini kwa kutumia tathimini ya maisha na baioanuai.

Tathimini hiyo inalenga kwenye uhusiano kati ya umasikini na mazingira na hususani katika kuchunguzi utegemezi na matumizi ya raslimali zinazotoka kwenye maeneo hayo kwa ajili ya maisha ya watu wa maeneo husika.

Warsha hiyo pia ililenga namna ya kubaini mazingira ya jumia ya kijamii na kiuchumi na viumbe hai ambavyo vinaishi katika vijiji hivyo; hali kadhalika kutafuta njia, namna na sababu za maliasili hizo zinavyotumika na matokeo ya matumizi hayo kwenye mazingira na hadhi ya kuhifadhi maeneo oevu, hali ya uchumi na mahitaji ya jamii.

Mradi wa Mtanza-Msona ulianzishwa kutokana na ufuatiliaji uliofanywa na Mpango wa Usimamizi wa Mazingira wa Rufiji wa Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na IUCN kutokana na maombi ya mashirika ya ambayo ni wabia za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)